**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 01/06/2022 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA**

**KU/SMC/BM/80/2022 – WALIOHUDHURIA:**

**A. WAHESHIMIWA MADIWANI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jastin Malisawa | - | Mstahiki Meya – Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Istus Kapufi | - | Naibu Meya |
| 3. | Mhe. Dimela Kafwa | - | Diwani viti Maalum |
| 4. | Mhe. Juma Mnanka | - | Diwani Kata ya Msua |
| 5. | Mhe. Adorfina Konongo | - | Diwani Kata ya Lwiche |
| 6. | Mhe. Frank Lupimo | - | Diwani Kata ya Milanzi |
| 7. | Mhe. Francis Manyika | - | Diwani Kata ya Majengo |
| 8. | Mhe. Mary Kipalasha | - | Diwani Kata ya Malangali |
| 9. | Mhe. Hadija Maufi | - | Diwani Viti Maalum |
| 10. | Mhe. Edwin Misasi | - | Diwani Kata ya Katandala |
| 11. | Mhe. Roswita Chekwe | - | Diwani Viti Maalum |
| 12. | Mhe. Janeth Sinyangwe | - | Diwani Viti Maalum |
| 13. | Mhe. Colnel Kafumu | - | Diwani Kata ya Sumbawanga |
| 14. | Mhe. Anthony Kayombo | - | Diwani Kata ya Chanji |
| 15. | Mhe. Gabriel Kimamala | - | Diwani Kata ya Izia |
| 16. | Mhe. Charles Chakupewa | - | Diwani Kata Ya Momoka |
| 17. | Mhe. Andrea Cheka | - | Diwani Kata ya Kizwite |
| 18. | Mhe. Juma Dawood Nzegere | - | Diwani Kata Mazwi |
| 19. | Mhe. Agustino Ngoani | - | Diwani Kata ya Ntendo |
| 20. | Mhe. Syriacus Pangani | - | Diwani Kata ya Kasense |
| 21. | Mhe. Cardius Mtullo | - | Diwani Kata ya Pito |
| 22. | Mhe. Leticia Kipeta | - | Diwani Viti Maalum |
| 23. | Mhe. Sangu Maarifa | - | Diwani Kata Mollo |
| 24. | Mhe. Anna Mwamba | - | Diwani Viti Maalum |
| 25. | Mhe. Lameck Pondamali | - | Diwani Kata ya Mafulala |

**B. WATAALAM**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Jacob J. Mtalitinya | - | Mkurugenzi wa Manispaa Katibu |
| 2. | Ndg. Frank Mateni | - | Afisa Maendeleo ya Jamii |
| 3. | Ndg. Andrew Zumba | - | Afisa Uchaguzi |
| 4. | Ndg. Eliud Fungo | - | Kaimu Afisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 5. | Ndg. Wema Mwashilindi | - | Kaimu Mchumi Manispaa |

6. Ndg. Joseph Nkonjera - Afisa Misitu
7. Ndg. Samson Medda - Afisa Utumishi na Utawala
8. Ndg. Thadeo Maganga - Afisa Maliasili na Utalii
9. Ndg. George Nyanga - Afisa Usafirishaji
10. Ndg. Deogratius Masalu - Kaimu Mkaguzi wa Ndani
11. Ndg. Robert Tarimo - Afisa Elimu Msingi
12. Ndg. Mussa Nginila - Afisa Manunuzi
13. Ndg. Fortunatus C. Lyapa - TSC
14. Eng. John Myovela - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi
15. Ndg. Jenifrida Manuma - Afisa TEHAMA
16. Ndg. Mathew Madama - Mwanasheria Manispaa
17. Ndg. Oswald Temba - Afisa Afya
18. Dr. Sebastian Siwale - Mganga Mkuu
19. Ndg. Richard Mkandarasi - Afisa Biashara Manispaa
20. Ndg. Piniel Mbura - Mweka Hazina
21. Ndg. Juliana Olumu - Kaimu Afisa Mazingira

**C: WAALIKWA**

1. Ndg. Sebastian Waryuba - Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga
2. Ndg. Neema Fungo - Jeshi la Akiba
3. Ndg. Sabina Mwajeka - Afisa Tarafa Itwelele
4. Ndg. Dafroza Msechu - Afisa Tarafa Lwiche
5. Ndg. Mohamed Mlumba - UHAMIAJI
6. Ndg. J. Mollel - Afisa Usalama Wilaya
7. SSP Maria D. Kway - Mkuu wa Polisi Wilaya
8. Ndg. Christina Mzena - DAS
9. Ndg. Melkior Komba - Magereza
10. Ndg. Tabu Shaaban - Katibu CCM Wilaya

| | | |
|---|---|---|
| 11. Ndg. Chami Chasuka | - | Mwenyekiti CCM |
| 12. Ndg. Elizabeth Simkway | - | Afisa Serikali za Mitaa |
| 13. Ndg. Ndg. James Mbungano | - | TAKUKURU |
| 14. Ndg. Baraka Lusajo | - | ITV |
| 15. Ndg. Sammy Kisika | - | AZAM TV |
| 16. Ndg. Edith Peter | - | VOS |
| 17. Ndg. Misri Mwasenga | - | STAR TV |
| 18. Ndg. Peter Helatano | - | Global TV |
| 19. Ndg. Musa Mwangoka | - | Mwananchi |
| 20. Eng. Samson Kelesi | - | TARURA |
| 21. Eng Emmanuel Kudema | - | TARURA |

**D. SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Maria Ntara | - | Katibu wa Vikao Manispaa |
| 2. Ndg. Lilian Konjani | - | Katibu wa Vikao |

**KU/SMC/BM/81/2022 – KUFUNGUA KIKAO:**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, Mwenyekiti alianza kwa kusoma dua. Mwenyekiti alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kutufikisha siku ya leo ambapo alisema kuwa kikao cha leo ni kikao cha Kawaida cha robo. aliomba wajumbe wazingatie kanuni katika kuchangia hoja katika kikao hiki. Mwenyekiti Alifungua kikao mnamo saa 4.00 Asubuhi

**KU/SMC/BM/82/2022 – KUTHIBITISHA DONDOO:**
Ziliwasilishwa dondoo za kikao cha tarehe 01.06.2022 wajumbe kwa kauli moja walizipokea na kuzithibitisha.

**KU/SMC/BM/83/2022 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MSTAHIKI MEYA NA MKURUGENZI**

**Hoja**
Mhe.Misasi alipenda kufahamu ni lini utekelezaji wa ujenzi wa stendi ndogo ya eneo la Makutano utakamilika.

**Jibu**
Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa ujenzi wa stendi ndogo ya Makutano ni mradi unaotakiwa kingizwa kwenye mpango kabambe kabla ya kuanza utekelezaji wake na suala hili amelipokea lakini linatakiwa kufuata utaratibu.

**KU/SMC/BM/84/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 11.03.2022**

Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa masahihisho ukurasa wa 5 kisha Katibu na Mwenyekiti waliuwekea saini Muhtasari huo.

**KU/SMC/BM/85/2022 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 11.03.2022**

Iliwasilishwa taarifa ya maazio ya kikao cha tarehe 11.03.2022 na wajumbe walipongeza kwa utekelezaji wake.

**KU/SMC/BM/86/2022 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI YA OKTOBA- DESEMBA 2021.**

**A. KAMATI YA UKIMWI**

Mwenyekiti wa kamati ya UKIMWI aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya UKIMWI kwa kipindi cha robo ya tatu ya Januari – Machi 2022.

Taarifa ilipokelewa

**B: KAMATI YA UCHUMI AFYA NA ELIMU**

Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi Afya na Elimu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Uchumi Afya na Elimu kwa kipindi cha robo ya tatu ya Januari– Machi 2022. Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

**Hoja**

Mhe. Cheka alipenda kufahamu kuhusu vigezo vinavyotumika kuchagua viongozi wa Wazee Maarufu.

**Jibu**

Mwenyekiti wa Kamati aliwaambia wajumbe kuwa Wazee wana uongozi wao kuanzia ngazi ya Mtaa hivyo ikitokea kuna shughuli yoyote wao wenyewe huchagua mwakilishi wa kuwawakilisha.

**Hoja**

Mhe. Kafumu alipenda kufahamu kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya Sumbawanga je kuna Fedha imetengwa kwa ajili ya mradi huo.

**Jibu**
Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa taarifa ya Kituo cha Afya Sumbawanga kinatakiwa kujengwa kwa hadhi ya Ghorofa kutokana na uhaba wa eneo hivyo Michoro imepelekwa Wizarani kwa ajili ya kupitishwa na pndi itakapo kamilika ujenzi utaendelea.

**Ushauri**

- Mhe. Misasi alishauri kuwa zoezi la kamata kamata watoto wa mitaani lihusishe ngazi zote katika Mitaa na Kata.
- Pia alishauri kijengwe kituo cha watoto wa mitaani.
- Mhe. Ngoani alishauri kuhusu utaratibu wa utoaji wa mikopo ya vikundi itolewe kwa Kata zote.

Tarifa ilipokelewa

**C: KAMATI YA MIPANGO MIJI**
Mwenyekiti wa kamati ya Mipango Miji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Mipango Miji kwa kipindi cha robo ya tatu ya Januari – Machi 2022.

**Hoja**
Mhe. Chakupewa alipenda kufahamu kuhusu mikakati ya Ofisi ya Mipango Miji kuhusu ujenzi horela unaonendelea hasa kwa Kata ya Momoka.

**Jibu**
Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa katika Kata kuna Uongozi ambao unapaswa kusimamia masuala yote yakiwepo ya Vibali vya ujenzi.

Taarifa ilipokelewa

**D: KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI**
Mwenyekiti wa kamati ya Fedha na Uongozi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya tatu ya Januari– Machi 2022, Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

**Hoja**
Mhe. Juma alipenda kufahamu je ni changamoto gani zilizo mkumba mzabuni wa uzoaji wa taka.

**Jibu**
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa changamoto alizokuwa nazo mzabuni ni kwamba hakuwa na mtaji wa kutosha na vifaa vya kutosha vya uendeshaji wa zoezi la uzoaji wa taka.

**Hoja**
Mhe. Mtollo alipenda kufahamu kuhusu vibarua wanao fanya kazi katika Stendi ya Katumba Azimio je ni lini malipo yaoyatashughulikiwa.

**Jibu**
Mweka hazina aliwaambia wajumbe kuwa ni kweli vibarua wanadai na ameanza kufanya utaratibu wa kuhakikisha madeni yao yanalipwa.

**Ushauri**

- Mhe. Mnanka alishauri kuwa Mapato ya tozo ya taka yaingizwe katika akaunti za Kata.
- Mhe. Kayombo alishauri kuwa kianzishwe Kiwanda cha kuchakata taka

Taarifa Ilipokelewa .

**KU/SMC/BM/87/2022 TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO**
Afisa Mipango Takwimu na Ufuatailiaji aliwasilisha taarifa ya Utekelezaji kazi Miradi ya Maendeleo kipindi cha robo ya tatu ya Januari - Machi 2022, wajumbe walichangia kama ifuatavyo:

**Ushauri**
Mhe. Mnanka alishauri kuwa Halmashauri isitegee Fedha za wahisani kuendesha miradi bali tuangalie mapato yetu ya ndani kwa ajili ya kuendesha miradi hiyo.

Taarifa Ilipokelewa.

**KU/SMC/BM/89/2022 – TAARIFA YA MSATHIKI MEYA**
Mstahiki Meya alimkaribisha Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliwashukuru wajumbe wa Baraza kwa michango yao mizuri pia alitoa msisitizo kwa maeneo yafuatayo.

- Manispaa iangalie namna ya uundaji wa timu ya Mpira wa Mguu
- Taarifa ya makisio ya mapato na makusanyo yakadiliwe kwa usahihi
- Halmashauri iweke mikakati kwa ajili ya suala la Watoto wa mitaani
- Halmashauri iweke mikakati ya uondoshwaji wa taka na namna ya kuanzisha kiwanda cha kuchakata taka.
- Afisa Afya kufanya ufuatiliaji eneo la Machinjio kuhusu usafi wa Mazingira ya kuchinjia na kuchunia ng'ombe

- Miradi yote ya Manispaa ikamilike kwa wakati na kufanya usimamizi wa kina katika utekelezaji wa Miradi.
- Uwepo utaratibu wa utunzaji wa Mazingira sambamba na upandaji miti katika maeneo ya makazi.
- Wananchi wahamasishwe kushiriki katika zoezi la Sensa

**Saalam za Chama Cha Mapinduzi Wilaya**

Mwenyekiti wa Chama alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na Afya anazotupatia pia aliomba Wataalam wahakikishe wanatekeleza maagizo ya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na kila mmoja kwenye sekta yake awajibike kutekeleza Ilani ya Chama.

**KU/SMC/BM/90/2022 – KUFUNGA KIKAO:**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo ina nia ya kuiletea maendeleo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 7.50 Asubuhi.

Umesambazwa na ……. Saini ……. Tarehe ……

**UMETHIBITISHWA / HAUKUTHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ……... | …….. |
| Jacob J. Mtalitinya | Mhe. Jastin Malisawa |
| **Mkurugenzi Manispaa** | **Mstahiki Meya** |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |